IBADA YA KILA SIKU

TOLEO LA 3

Septemba 2022

# HabariNjema

KILA SIKU

**BURE**
HAKIUZWI
KITABU HIKI CHA IBADA KIMESHALIPIWA NA WASHIRIKA WETU ILI KISAMBAZWE BURE

KAMA VILE MAJI YA BARIDI KWA MTU MWENYE KIU, NDIVYO ILIVYO HABARINJEMA ITOKAYO KATIKA NCHI YA MBALI. [MITHALI 25:25]

Uebert & BeBe
ANGEL




## UEBERT & BEBE ANGEL

Wakiwa na miaka mingi ya kufanya huduma ya Mungu, Uebert na Bebe Angel ni mapainia na sauti zinazoongoza kwenye kutangaza habari njema ya neema ya Mungu (Euangelion) pamoja na unabii duniani kote.Kwa pamoja ni waandishi bora wa vitabu kama Habari Njema, Intimacy, Prayer Banks, Supernatural Power of the Believer n.k. Uebert na Bebe Angel ni wazungumzaji wanaotafutwa kwenye mikutano sehemu mbalimbali duniani, ni viongozi wa kidunia.

Wanatambulika na kuheshimika kwa maono yao, uvumbuzi na ujasiri wao. Kama waanzilishi wa Kanisa la Good News (Spirit Embassy), na wenye ofisi ya kinabii, wamegusa maisha ya mamilioni ya watu ulimwenguni kupitia mapenzi yao ya kuvuna nafsi na kuleta ufunuo wa habari njema ya neema ya Mungu (Euangelion).


GoodNews
Become a
GoodNewsWorld
PARTNER
Your MiracleTV
IS EXPANDING
YOU CAN NOW WATCH
I AM NOT ASHAMED
PARTNER NOW AND HELP SPREAD
THE GOODNEWS AROUND THE WORLD
VISIT www.goodnewsworld.com/ partner



**Isaya 26:3 (NEN)**
**"Utamlinda katika amani kamilifu yeye ambaye moyo wake ni thabiti, kwa sababu anakutumaini wewe."**

Tunaishi katika ulimwengu ambamo ni vigumu sana kuipata amani tu,achilia mbali ''amani kamili''. Kila mara tunapowasha redio, televisheni au kutumia jukwaa lolote la mitandao ya kijamii, matukio ya sasa ambayo yanazuka ni ya huzuni tu na hakuna chochote ambacho kitampa mtu wa kawaida motisha au kumtia moyo kukubali kwamba maisha ni mazuri kama yalivyoumbwa na Mungu. Maandiko yetu ya leo yanatoa mpaka fulani kati ya wale ambao mioyo yao ni thabiti kwa sababu wanamtumaini Mungu. Kwa hiyo, Mungu huwaweka salama katika amani yake ambayo ni kamilifu.

Kuna wengine ambao akili zao na mchakato wa mawazo ni utupu kabisa havina Mungu. Kumbuka kwamba tuko katika ulimwengu huu lakini si wa ulimwengu huu, hii inahusisha kwamba chochote tunachofanya kama Wakristo kinapaswa kumuakisi yule tunayemwakilisha. Biblia inatuambia: ''Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ,ambayo ilikuwamo ndani ya Kristo Yesu:'' ( Wafilipi 2:5 ) , nia ya Kristo haifurahii msongo wa mawazo wala masononeko ya moyo. Nia ya Kristo haisumbuliwi na matukio ya sasa wala kufadhaika unapokabiliwa na hali ambazo unafikiri haziwezekani.

Maandiko ya leo yako wazi kabisa kwamba, moyo wako unapoelekezwa kwa Mungu, hakuna kinachoweza kukuyumbisha bila kujali ni hali gani, Mungu mwenyewe atakulinda . Kwa maneno mengine, ulinzi na usalama unaoutafuta unaweza kupatikana kwa Mungu pekee. Kumtumaini kwako Mungu kunatokana na neno lake lenye ahadi zake nyingi kuhusu wewe. Soma neno lake kila siku !

## UKIRI WA KINABII

**Amani yangu ni amani ya Mungu isiyoweza kuharibiwa, popote niendapo naibeba amani ya Mungu. Maisha yangu ni dhihirisho la amani ya Mungu inayotoka ndani yangu. Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI:** Wafilipi 4:6-7



**2 Wakorintho 3:2**
**"Ninyi ndinyi barua yetu, iliyoandikwa mioyoni mwetu, inajulikana na kusomwa na watu wote:"**

Mstari wa leo unaashiria kitu kilichoandikwa, barua, kijitabu, kipeperushi, kijarida vyote hivi vina kitu sawa, yaani vyote vinabeba taarifa. Sote tunaweza kusoma kitu kilichoandikwa ndani yake; lakini tunawezaje kusoma kitu kilichoandikwa katika moyo wa mwanadamu? Ili kupata ufahamu wa kusoma yaliyo ndani ya moyo wa mtu, Biblia inatuambia kwamba ''...mtu mwema katika hazina njema ya moyo wake, hutoa yaliyo mema.. . '' (Luka 6:45). Unapoonekana mahali fulani na ukawa kimya, hakuna mtu anayeweza kujua kama wewe ni mwenye busara au mpumbavu. Inachukua maneno machache kutiririka kutoka kwenye midomo yako na watu kutambua hekima au upumbavu wako.

Ulichoweka akiba moyoni mwako linapokuja suala la Neno na maarifa ya Mungu, kitamwagika pale unapoanza kunena. Ukiungwa kwenye neno, ukajaa neno, na kuzama ndani ya neno, popote uendapo, kile ulichoundwa kwacho kitaonekana kwa wengi. Mtindo wako wa maisha haujafungwa tu kwenye huduma ya kanisa, lakini unaenda zaidi mpaka sokoni , mahali pa kazi, chuo kikuu chako, machapisho yako ya kwenye mitandao ya kijamii na majukwaa a kijamii ,na mikusanyiko ya kifamilia. Unachosema na kufanya huko nje kinapaswa kuwa pendekezo la kuwavuta wengi kwa Kristo . Wewe ni jengo na kwa hivyo , maisha yako yanapaswa kuwa sumaku ya kuvutia umati kwa BWANA wetu bila kumbakisha hata mmoja.

## UKIRI WA KINABII

**Maisha yangu yamekusudiwa kung'aa zaidi katika ulimwengu huu wa giza. Ninapozungumza, maneno yangu yatakuwa yamejaa hekima ya Roho Mtakatifu. Mimi ni Mbeba Habari Njema. Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Wakorintho 9:2



**Waefeso 3:20**

**"Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu;"**

Huwa nashangaa mara nyingi watu wanaponiuliza jinsi nilivyoweza kupenya hadi kwenye asilimia ndogo ya juu ya wale walioorodheshwa kwenye Jarida la Forbes. Siku zote huwa nawaambia kwamba thamani yangu inaamuliwa na kile ninachosema nina thamani na sio tu kwa takwimu zilizotolewa na watu. Ukisoma mstari huo, utaona kwamba Mungu anaweza, yaani anafanya kile anachosema. Zaidi ya hayo, inaweza kusemwa kwamba uwezo Wake ni wa kupita kiasi na umeelezwa waziwazi hapa, unazidi uwezo wetu wa kufikiri kwetu. Tatizo la Wakristo wengi hawajua utele unaohusishwa na madhihirisho wa nguvu za Mungu.

Unapoweka kikomo juu ya nguvu za Mungu katika maisha yako, hicho ndicho kiwango cha nguvu za Mungu utakutana nacho na kupokea. Unapoondoa mipaka na kujua kwamba yeye ni Yehova El Shaddai, "Mungu mwenye maziwa mengi" ndipo utagundua kwamba uwezekano wake wa kuingilia kati maisha yako hauna kikomo. Nguvu zake zipo kufanya kazi ndani yako na kupitia wewe, hivyo anza kutumia kiwango hiki kisicho na kikomo cha nguvu za Mungu zinazofanya kazi ndani yako leo na utafanya mambo makuu kwa ajili yake. Acha kujiwekea mipaka , Mungu anaposema nawe, anaweza kufanya kile alichosema kwa jina la Yesu.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni nyumba ya Nguvu za Mungu, siwezi kuwekewa mipaka, ushujaa wangu hauna kikomo kwa kadri ya uweza wake unaofanya kazi ndani yangu kila wakati. Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**

Warumi 16:15



**1 Wathesalonike 5:12-13**
**"Lakini ndugu, tunataka muwatambue wale wanaojitaabisha kwa ajili yenu, na kuwasimamia ninyi katika Bwana, na kuwaonyeni; mkawastahi sana katika upendo kwa ajili ya kazi zao."**

Mengi ya yale tunayoyaona leo makanisani yanapungukiwa sana na yaliyosemwa kwenye maandiko haya. Mtume Paulo anawaonya washiriki wawastahi sana wale waliowekwa juu yao kama manabii, mitume , wachungaji, wainjilisti ,na waalimu. Heshima inaenda zaidi ya ofisi zilizotajwa, hata wale walio na nyadhifa kuu katika Kanisa wanahitaji kuheshimiwa sana kwa ajili ya kazi zao.

Kwa nini Mtume Paulo anaona kuwa ni muhimu sana kutaja kwa uzito jambo la kuwaheshimu viongozi waliowekwa juu yako? Ni lazima ifahamike kwamba upako wa Mungu hauwezi kubatilishwa. Unapokutana na mpakwa mafuta wa Mungu kiwango chako cha utii, unyenyekevu ,na heshima kwao kitachochea upako waliobeba kufanya kazi kwa ajili yako. Wakristo nwengi wenye roho ya Wanikolai wanajificha kwa kuiigiza na wakati fulani wanapiga magoti mbele ya mtumishi wa Mungu huku mioyo yao ikiwa imesimama kwa kiburi sana, na wanatarajia upako kuwafanyia kazi. Hii haiwekani kabisa! Upako unapounyenyekea,kuwa mtiifu kwa huo,na kuuheshimu hakika utakufanyia kazi. Wakati unapoamua kuwaheshimu bila masharti wale waliowekwa juu yako katika uongozi, haraka utaona maisha yako yakichukua mkondo wa kwenda juu katika jina kuu la Yesu.

## UKIRI WA KINABII

**Ninachagua kwa makusudi sasa kuwaheshimu na kuwatii wale waliowekwa juu yangu. Maisha yangu yataakisi Kristo ndani yangu kila siku na yatang'aa popote niendapo kwa jina la Yesu, Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Wakorintho 16:18



**Yohana 6:29**
**"Yesu akajibu, akawaambia, 'Hii ndiyo kazi ya Mungu, mmwamini yeye aliyetumwa na yeye"**

Unapowauliza Wakristo wengi ni, nini mpangilio wa vipaumbele katika orodha ya Mungu ya mambo ambayo ni muhimu sana kwa moyo wa Mungu? Labda wengi watajibu ''kuvuna nafsi''. Ukweli wa mambo ni tofauti. Kwa kadiri Mungu anavyojali sana Kuvuna nafsi, lakini kilele cha orodha ya Mungu ni: Kuaminiwa. Kiini cha uhusiano wa Mungu na mwanadamu siku zote huanza na Mungu akihesabu ikiwa unamwamini au la. Ikiwa utamkubali Mungu sawa na neno lake au la. Kwa Mungu, hakuna kuwa katikati au au kutofungamana na upande wowote. Ilimpasa Mungu kumchunguza Ibrahimu mara mbili mbili, juu ya hili pale alipomwambia aende kumtoa dhabihu mwanawe wa pekee Isaka; kwa uhakika kiasi kwamba mpaka Abrahamu alipokuwa karibu kabisa kufanya hivyo, ndipo Mungu alilazimika kumzuia. Biblia inaweka hivi: ''Abramu akamwamini (aliyemtumainia, akamtegemea, akadumu kwa) BWANA; naye kwake hili likahesabiwa kuwa haki'' (Mwanzo 15:6).

Unaona jinsi Mungu anavyoangalia suala kumwamini yeye, anaiweka kwenye mizania ya mbinguni na kuiweka kwenye hesabu yako kama haki. Huyu ndiye aina ya Mungu tunayemwabudu, ambaye shauku yake ni sisi 'kuamini katika Yeye.Unapomthibitishia Mungu kwamba unamwamini, unajua kwa hakika kwamba salio lako la benki hubadilika automatiki.

## UKIRI WA KINABII

**Ninamwamini Mungu! Sasa ninamtumaini Mungu kwa utu wangu wote; roho, nafsi ,na mwili. Maisha yangu hayatakuwa sawa tena. Amina !**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mithali 3:5

# SI KWA UWEZO, WALA SI KWA NGUVU



**Zekaria 4:6**
**"Akajibu, akaniambia, akisema, 'Hili ndilo neno la BWANA kwa Zerubabeli, kusema, si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa Roho yangu, asema BWANA wa majeshi."**

Maandiko haya mara nyingi yamenukuliwa miongoni mwa waamini , lakini ni wachache sana ambao huelewa maana yake kwa undani. Neno ''uweza'' hapa ni neno la Kiebrania ''chayil'' linalomaanisha ''nguvu au kani" iwe ya watu/ jeshi au rasilimali nyingine kama mali na utajiri. Pia, neno ''nguvu'' kutoka neno la Kiebrania ''koach" maana yake "kuwa imara au mwenye nguvu". Nabii Zekaria alikuwa akizungumza yale ambayo Mungu anamwambia Zerubabeli ambaye alikuwa amerudi kutoka katika utumishi wa kifalme kwa mfalme katika nchi ya kigeni na sasa alikuwa akisimamia mradi wa kujenga upya kuta za Yerusalemu zilizovunjika.

Bidii na shauku ya Zerubabeli kutekeleza mradi huu kama ilivyovuviwa na Mungu haikumuepusha na mashambulizi ya maadui. Vita vilivyokabili katika kusimamisha kuta za Yerusalemu vilikuwa vya kudumu, mashambulizi ya kila siku. Wajenzi walishika silaha za vita kwa mkono mmoja na kutumia mkono mwingine kuendeleza mradi huo. Hii inatufundisha kama Wakristo kwamba hatuko huru kutokana na mashambulizi ya adui . Wakati mwingine inakuwa mbaya zaidi pale unapoweka, kiapo cha utii wako kwa Kristo . Njia pekee ni kuwa na ushirika zaidi na Roho Mtakatifu na kwa kufanya hivyo, Roho Mtakatifu atashughulikia matatizo, na ushindi wako unalazimika kuchipuka kwa muda mfupi pale Roho Mtakatifu anapochukua hatamu. Wewe ni mshindi katika Kristo!

## UKIRI WA KINABII

**Ninakaa ndani ya Mungu kama yeye anavyokaa ndani yangu. Siwezi kushindwa maishani kwani Roho Mtakatifu ndiye Mshirika wangu Mkuu. Maisha yangu yatavutia Habari Njema kila dakika ya siku na ushindi wangu umehakikishwa katika Kristo. Amina**

**MAFUNZO ZAIDI**
Hosea 1:7



**Wafilipi 1:7**
**" Vilevile kama ilivyo wajibu wangu kufikiri haya juu yenu nyote; kwa sababu ninyi mmo moyoni mwangu; kwa kuwa katika kufungwa kwangu, na katika kazi ya kutetea Injili na kuithibitisha, ninyi nyote mmeshirikiana nami neema hii."**

Loo! ni andiko lenye nguvu kama nini! Mwisho wa andiko hili unasisitiza kifungo cha ndani sana cha ushirika wa neema. Unakuwa mshiriki wa neema iliyo juu ya mtu pale unapokuwa mamoja na ufunuo wao wa neno na maono. Ushiriki wako kwenye yale yanayomuhusu, kujali kwako maisha yake ya kila siku, huduma yake, utume wake uwe wa ndani au kimataifa, maono yake hasa linapokuja suala la kueneza Injili, utetezi na uthibitisho wa injili nikiweza kwa kiasi fulani kunukuu, kutoka katika maandiko kama Paulo anavyo andika. Watu wengi katika mazingira ya Kanisa kwa makusudi hukataa kushiriki katika huduma yoyote iwe ya kifedha au vinginevyo, lakini wanatarajia kupata mavuno mengi! Je, unatarajia kuvuna katika ulimwengu gani ambapo hukupanda?

Kama muumini , utaepuka uvivu na kutaka kuwa na kushiriki kikamilifu katika huduma. Ili kuwa mshiriki wa neema inadai kuwa na bidii katika karibu kila eneo la kazi ya huduma na uwanja wa umisheni wa Mwenye Maono. Unapoanza kufanya hivi, basi unakuwa na haki ya kisheria ya kiroho ya kuweka madai ya kupata manufaa ambayo huja kama furushi la neema juu ya maisha mtu wa Mungu. Ni ufunuo wao unaouishi.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mshiriki wa neema ya Mtumishi wangu wa Mungu! Kiwango cha kujitoa ninachotumia katika kufungua pakacha la neema kitaamua kufunuliwa kwangu kama mshirika. Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 15:27



**Warumi 8:37**
**"Lakini, katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda."**

Unahitaji kuelewa kwa makini sababu na mazingira ya andiko hili kabla ya kupata kwa uwazi maandishi ya maandiko. Maandishi yalianza na neno ''lakini'', ambalo ni ''alla'' katika Kiyunani ambalo yanahusisha maneno kama ''pamoja na hayo", ''hata hivyo'', ''lakini" . Mwandishi wa kitabu cha Warumi, Mtume Paulo ndiye mwenye mamlaka sahihi ya kufundisha juu ya ushindi na kufanya mateka kutoka kwenye mtazamo wa mwamini. Paulo alivunjikiwa meli, akaumwa na nyoka mwenye sumu kali, akawekwa gerezani mara nyingi sana, na akapigwa na askari wa Kirumi waliokuwa makatili sana katika kipindi hicho, lakini katika haya yote Paulo anazungumza kwa ujasiri kwamba sisi ni zaidi ya washindi kwa njia ya Kristo aliyetupenda.

Mtu anaweza kujiuliza ikiwa Kristo anatupenda, kwa nini nipitie magumu haya yote? Kwa nini biashara yangu haijainuka kama nilivyopanga? Kwa nini familia yangu inasambaratika? Kutakuwa na kwa nini nyingi sana! Hebu tufikie kiini cha jambo kama Paulo asemavyo: ''... tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda'' (warumi 8:37). Ili kuwa mshindi ni lazima upitie angalau vita, na kuwa zaidi ya mshindi huashiria kuwa umeshinda vita vingi sana. Kwa nini hizo zinajibiwa katika andiko hili linalohusisha ushindi wako na Kristo ambaye anakupenda. Kristo anapokuwa ndani yako na wewe ndani ya Kristo, hiyo ndiyo uthibitisho kwamba ushindi wako umehakikishwa. Tangu sasa, acha kufanya vita kwa nguvu na uwezo wako. Biblia inasema hivi ''.... Kristo ndani yetu, tumaini la utukufu" (Wakolosai 1:27)

## UKIRI WA KINABII

**Niko ndani ya Kristo na Kristo ndani yangu; kwa hivyo, ushindi wangu ni umehakikishwa. Nitaishi kila wakati juu ya changamoto zangu. Siondoshwi na vile wengine wanavyofikiri kunihusu, kwa maana najua, Kristo ndani yangu ndiye tumaini la utukufu. Amina!**

**MAFUNZO ZAIDI**
2 Mambo ya Nyakati 20:15



**Waefeso 5:18**
**“Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho;”**

Wengi wasio Wakristo au wale wakristo wa kwenda kanisani tu wanaweza kuwa na tabia hii pia: kulewa kwa mvinyo au aina fulani ya mchanganyiko ili wafikie kwenye kwenye kiwango cha msisimko na shangwe. Wanauchukulia kwa uzito ulevi huu kwa divai kuleta wazimu au wingi wa furaha na kuwafanya wasahau wasiwasi au shida zao kwa muda. Maandiko ya siku ya leo yanaonya dhidi ya aina hiyo ya furaha . Baadhi ya matoleo ya Biblia yanasema inakupelekea kwenye ufisadi kwa sababu itaharibu maisha yako huku tafsiri nyingine ikiita “upumbavu”. Sasa tunaweza kuona wazi kwamba si jambo la kupendeza kulewa kwa mvinyo.

Kwa upande mwingine, katika andiko hilo hilo, kuna aina chanya ya ulevi ambayo inatengenezwa na Roho Mtakatifu. Aina hii ya ulevi katika Roho, haitachochea matendo ya kipuuzi. Unapolewa katika Roho, atakuongoza kufikiri vyema kwa hekima ya hali ya juu isiyo ya ulimwengu huu. Katika hali ya ulevi katika Roho, kuna kutiwa nuru, ambapo uwezo wako wa kufikiri huanza kupata ufunuo kutoka kwa chanzo kitakatifu kinachoongozwa na Roho ambapo Mungu ataanza kukufunulia siri na ajabu zake . Manabii wa kale walielewa hili kwa uwazi, muda hadi muda walitaja katika Biblia, kwamba mambo waliyoandika walipewa walipokuwa katika Roho, au kwa urahisi walipokuwa wamelewa Roho.

## UKIRI WA KINABII

**Ninachagua kujazwa na Roho Mtakatifu na nitazidi hekima ya kawaida ya wanadamu. Mtindo wa maisha na tabia yangu vitadhihirisha uwepo wa Mungu kwa sababu nimejazwa na Roho. Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mithali 23:31



**Ufunuo 22:12**
**"Tazama, naja upesi, na ujira wangu u pamoja nami, kumlipa kila mtu kama na kazi yake ilivyo"**

Nilichukuliwa Mbinguni katika mojawapo ya ziara zangu nyingi katika Roho; na Bwana, Yesu aliniambia, ''Waambie watu wangu, naja upesi.'' Nilijibu kwa kusema, ''Bwana, nawaambia". Najua hili litakuwa jambo la kawaida kwa watu wengi, kwa sababu wanafikiri wanajua kila kitu. Mojawapo ya mambo yanayonipata baada ya maono haya, ni kwa nini Bwana anipe neno hili maalum?

Nimekuwa nikipiga kengele tangu zamani kwamba sisi ni enzi ya mwisho na sasa tunaishi mwishoni kabisa mwa ukurasa. Kama mechi ya kandanda, sasa ni kipindi cha neema ambacho kwa kawaida wanakiita muda wa ''majeruhi''au muda wa ''ziada" .Sio wakati tena wa kucheza ukiwa Mkristo. Ni wakati wa kuchukua mambo ya Mungu kwa uzito . Ninawaambia watu kila wakati , kwamba huduma ni kazi ya kudumu, mambo mengine yote ni ya muda mfupi.

Kama mchezaji wa mpira wa miguu, unapojua kwamba mechi sasa inakaribia kwenye ''dakika za nyongeza'', utakuwa na ufahamu wa ukweli, kwamba filimbi inaweza kupulizwa na mwamuzi wakati wowote ambao itamaliza mchezo. Unapoamua sasa kuchukulia mambo ya Mungu kwa uzito , basi Mungu atachukua mambo kukuhusu wewe kwa uzito ule ule. Hebu hii iwe mtazamo wako kwamba HAKUNA MUDA ULIOBAKI! Unyakuo unakaribia sana!

## UKIRI WA KINABII

**Niko tayari kunyakuliwa; maisha yangu sasa yamefokasi kwa Mungu. Nitafuata maagizo ya Mungu na kupata mashauri katika NENO lake. Mimi ni wa mbinguni,na adui hawezi kuyakatisha tamaa maisha yangu. Amina!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Isaya 40:10

# MUNGU NI MWAMINIFU



**1 Wathesalonike 5:24**
**"Yeye mwaminifu ambaye awaita, naye atafanya"**

Mungu anatoa wito hapa. Amesema mara nyingi kwenye Neno lake kwamba uaminifu wake wadumu. Biblia kwenye (Zaburi 89:33) pia inasema, ''Wala sitafanya uaminifu wangu kuwa uongo''. Udhaifu wa ubinadamu wetu unatuwekea giza katika maaamuzi yetu ambapo tunauumba ulimwengu wetu katika namna tunavyomfikiri Mungu kuwa ndivyo alivyo.

Tunamwazia Mungu kama vile ametibuliwa sana na kukasirika na kutuchukia kwa sababu tunaweza kuwa tumekosea mahali. Kinyume chake, Mungu alipokuita, tayari kulikuwa na mpango na kusudi la Mungu alilokuwa amekutengenezea. Katika huduma, Mungu anapokupa maono, hukupa kila kitu cha kutekelezea maono hayo. Unapokuwa katika huduma na kila mara unang'ang'ana na mahitaji, basi kuna haja ya marekebisho kwenye maono yako.

Mungu katika upangaji wake wa Ki-Ungu tayari alikuwa ameyanasa maisha yako yote, lakini wakati mwingine hulka zetu za kibinadamu na asili hutufanya tugeuke na kujaribu kuiruka ajenda ya Mungu . Watu wengi hufikiri kwamba, Mungu anachukua muda zaidi na yupo pole pole kutenda, na katika mchakato huu wanakabiliana na changamoto za maisha zinazowachochea kulitukana jina la Mungu. Iwapo moyo wako na mawazo yako yatashikamana na Neno la Mungu na Roho Mtakatifu, ataanza kukufundisha, utaona maisha yako yakichukua mkondo wa juu unapotembea katika mipango ya Mungu. Ifanye kuwa sehemu ya kujua kwamba kabla Mungu hajakuita, tayari alikuwa amepanga maisha yako. Mungu anapoita , atakupatia mahitaji yote!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni Mkristo mtoa uthibitisho niliyeitwa kwenye ukuu. Ninatembea katika mipango mitakatifu ya Mungu kwa maisha yangu na sitachepuka njiani. Kutembea kwangu na Mungu kutaumba ndani yangu maarifa na nguvu za kutenda Maajabu yasiyo na Idadi . Haleluya!**

## MAFUNZO ZAIDI

Wafilipi 1:6



**1 Wakorintho 11:1**
**"Mnifuate mimi kama mimi ninavyomfuata Kristo."**

Mtume Paulo aliandika theluthi moja ya Biblia na kwa yeye kusema kwa ujasiri kwamba Kanisa la Korintho linapaswa kumfuata yeye kama anavyomfuata Kristo; itachukuliwa tofauti na watu wengine ,haswa wakati wa kuleta somo hili kwa watu makanisani ambamo wanadhani wanajua zaidi na bora.

Ninaposema baba yangu wa kiroho, Mchungaji Dk. Chris Oyakhilome ni nyota wangu, watu wengi huko nje watakuwa na tafsiri zao wenyewe. Hakika namuiga Mchungaji Chris anaponifungulia maandiko kwa ufunuo wa juu zaidi. Mchungaji Chris aliponiombea kwa maombi rahisi, kwamba "ufunuo wa neno Mungu uongezeke ndani yangu", tangu wakati huo na kuendelea, Neno kutoka kwenye maandiko lilitoka ndani yangu likiwa hai na kudai kunenwa. Baba yangu wa kiroho, Mchungaji Chris ana bidii kubwa juu ya Yesu na Neno la Mungu ,kusema tu kwa uchache, kanisa lake linaweza kuhesabu kusanyiko lake ulimwenguni kote kwenye mabilioni ya watu. Linajulikana na karibu kila kaya kwenye sayari hii, unawezaje kutoiga jambo kama hilo!?

Nashangaa unamfuata nani kama kielelezo anapomfuata Kristo? Je! ni mtu anayeweza kukuwajibisha na kusema maishani mwako kama vile baba anavyozungumza na mwanae? Biblia imejaa mahusiano ya baba na mwana kama vile Paulo kwa Timotheo, Eliya kwa Elisha, na watu hawa waliongezeka kwa sababu ya wale walio juu yao katika Bwana.

## UKIRI WA KINABII

**Macho yangu yameelekezwa kwenye mambo yaliyo juu. Sisombwi na waharibu na walaghai. Maisha yangu ni kazi bora, ya kutisha na ya ajabu, iliyounganishwa na viungo wangu kukusanya mikusanyiko yangu. Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Waefeso 5:11



**Warumi 13:1**
**“Kila mtu na aitii mamlaka iliyo kuu; kwa maana hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu; na ile iliyopo imeamriwa na Mungu”**

Ninashangaa sana jinsi Wakristo wanavyowatendea watu katika Uongozi, iwe Kanisani au kiraia. Hebu tuanze na nyumba ya Mungu ambako imekuwa dhahiri kwamba heshima ya kweli sasa ni vigumu sana kuipata katika kanisa. Viongozi wa kanisa wanaopaswa kuheshimiwa kwa heshima kubwa, hutendewa kikawaida na bila heshima inayostahili hata miongoni mwa washarika wao wenyewe.

Je, unatarajiaje kubarikiwa na Mungu wakati unapuuza mamlaka aliyoweka juu yako? Maandiko ya leo yana ujasiri sana kusema kwamba, tawala zote (mamlaka) zimewekwa na Mungu. Inamaanisha, Mungu anaruhusu mamlaka hiyo kuwa juu yako kwa sababu fulani. Mpaka au vinginevyo ujifunze kuheshimu viongozi wako bila kujali umri wao, kiwango chako cha juu cha kuinuliwa kinaendelea kusubilishwa na hujui ni kwa nini .

Ikiwa unaelewa kwamba Mungu anathamini sana heshima na utii, utaona mabadiliko kwenye maisha yako binafsi unapotembea katika mwendo huu. Namna unavyowaheshimu wale walio na mamlaka juu yako, itaamua kiwango chako cha kuinuliwa. Biblia imejawa na kumiminika kwa baraka juu ya wale wanaoheshimu mamlaka zao za kiroho. Unapotaka kuheshimiwa na kukuzwa, ujizoeze kuheshimu wengine.

## UKIRI WA KINABII

**Kupitia Kristo, nina hekima ya kuheshimu mamlaka iliyo juu yangu. Najua kwa kuwaheshimu wengine; Mungu ataniheshimu na kunizidisha. Heshima itakuwa kipimo changu kwa Mungu, kwa mamlaka na kwa wengine kuanzia sasa na kuendelea. Haleluya**

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Petro 2:13



**Kumbukumbu la Torati 2:25**
**"Hivi leo nitaanza mimi kutia utisho wako na kuhofiwa kwako juu ya watu walio chini ya mbingu na kila mahali, watakaosikia uvumi wako,na kutetemeka na kuingiwa na uchungu kwa sababu yako."**

Je, umefurahia, ndugu hapo? Andiko hili linakuambia kuwa uwepo wako tu utamkasirisha mtu na kumsababishia maumivu ya kichwa kwa sababu tu ya wewe ni nani. Unapoonekana kwenye eneo, utakuwa mshawishi na kile unachosema kitabeba uzito na nguvu. Hivi ndivyo ulivyo katika Kristo. Kiongozi fulani wa taifa alisikia kuja kwangu, nchini kwake hufanya mikutano wa nje ambayo ilipangwa kwa muda mrefu kabla ya ujio wangu, na kila mtu alifurahi kunipokea isipokuwa mkuu wa nchi ambaye hakuwa na furaha. Nilipofika katika nchi hiyo, mara nikasimamishwa kwenye uwanja wa ndege na kukataliwa kuingia, sababu iliyotolewa, ilikuwa Raisi huyo hakutaka uwepo wangu.

Nilijua nguvu fulani zilikuwa zikiathiri uamuzi wa Raisi wa nchi hiyo ambaye alinikatalia kuingia, kwa hivyo kabla ya kuondoka; Niliamuru na kutangaza kwamba Raisi huyo hatapata muhula wa pili wa kuongoza, na ikawa hivyo! Alishindwa katika mchakato wake wa kuwania muhula wa pili wa uraisi. Nguvu uliyo nayo ndani ya Kristo haiwezi kufikirika! Unaweza kuzungumza na kubadilisha tawala, Je? si zaidi sana kwa hali za kawaida kawaida, unapozungumza jambo, litatimia. Kuwa jasiri na utamke na utashuhudia matokeo yanayoonekana katika jina la Yesu!

## UKIRI WA KINABII

**Neno la Mungu litachukua nafasi ya kwanza juu ya ripoti yoyote inayonihusu. Natembea katika afya ya Ki-Mungu, naripoti habari njema, maneno ninayozungumza si matupu bali yanabeba nguvu! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Kutoka 23:27



**2 Timotheo 3:1**
**"Lakini ufahamu neno hili, ya kuwa siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari"**

Kwa kudokeza, kuchanganua maandishi haya , tutaangalia kwa makini maneno ya mwanzoni mwa aya ili tuelewe muktadha wake. ''Lakini ufahamu neno hili……'' linapendekeza kwamba kuna kitu kimesemwa tayari na hii ni nyongeza kwa taarifa iliyotangulia. Tunaishi katika enzi ya mwisho ambapo tunashuhudia kila siku ghasia zikiongezeka kwa kiwango ambacho hakijawahi kuonekana katika ustaarabu uliopita. Kila chanzo cha habari, mitandao ya kijamii, vyombo vya habari vya kawaida vimejaa vichwa vya habari kuhusu ghasia. Jambo la kusikitisha, wakati mwingine ni kwamba tumeshuhudia kwa macho yetu vitu hivi, kwani vinatangazwa moja kwa moja kutoka kwa eneo lolote ulimwenguni. Watoto hukabiliwa na vitendo vya kikatili na unyanyasaji mkubwa ambavyo vinaonyesha mmomnyoko wa maadili wa jamii katika kiwango cha juu kabisa.

Hata hivyo, cha kushangaza, mengi ya mambo haya ya kipumbavu yameidhinishwa na watu tunaowakabidhi ofisi za umma. Mitaala katika mashule inabadilishwa sana ili kuhalalisha na kuuhubiri uozo wa maadili kana kwamba ni jambo la kawaida. Hakika hizi ni nyakati za hatari na kwa hakika huashiria ''siku za mwisho''. Ulimwengu ulioko huko nje, unajaribu sana kuzuia na kunyamazisha kila sauti ya kimaadili inayozungumza juu ya kiwango cha Kii-Mungu. Nyakati hizi za hatari zimefika, huhitaji kuambiwa jinsi unavyoona mambo haya yakitendeka mbele ya macho yako mchana kweupe. Maisha kama tunavyojua yatakoma kwa ghafla wakati wowote kuanzia sasa, hii si la kukutisha bali ni kukutayarisha. Huu ni wakati uliowekwa wa kuwa na ujasiri na kuhubiri Habari Njema ya Kristo kwa kila kiumbe!

## UKIRI WA KINABII

**Najua nguvu ya kushinda dhambi na majaribu inakaa ndani yangu. Siwezi kuendana na viwango vya ulimwengu huu. Maisha yangu yatamdhihirisha Kristo ndani yangu popote niendapo . Siwezi kunyamazishwa;sauti yangu itafanya mabadiliko katika ulimwengu wa machafuko! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI:** 1 Timotheo 4:1



**Isaya 40:31**
**"Bali wao wamngojeao BWANA watapata nguvu mpya; watapanda juu kwa mbawa kama tai; watapiga mbio, wala hawatachoka; watakwenda kwa miguu, wala hawatazimia."**

Inafurahisha kwamba andiko hili linalinganisha maarifa ya Ki-Mungu uliyonayo kama namna ya nguvu inayomfanya tai kupaa juu. Tai ana sifa kadhaa ambazo zinajumuisha; tai hajisalimisha kwa adui yake, atapigana hadi mwisho bila kujali ukubwa wa adui. Kwa nini, maandiko yanamlinganisha mwamini na tai ? kirahisi kabisa, ni kwa sababu ya uvumilivu na ukakamavu ambao ni muundo wa kinasaba wa tai, ambacho kinapaswa kuwa sawa na mwamini aliyejazwa na Roho . Sifa hizi kuu za tai zinapaswa kumfanya muumini kuelewa kwamba kuna kitu maalum kumhusu yeye. Huwezi kuondoshwa kwa urahisi wakati hali mbalimbali zinainua vichwa vyao vibaya dhidi yako. Kama tai, bila kujali saizi, au umbo, ushupavu wako wa kushikilia na kuvumilia hadi ushindi, lazima liwe lengo pekee lisilo na mbadala.

Wakristo wengi hukata tamaa haraka sana tena kwa urahisi sana na kufikia muafaka bila kuzingatia sana tabia na asili ya Kristo. Wakati tufani inapowajia, wataanza kulalamika na kufikiria ulimwengu wote umepanga njama dhidi yao. Daudi hakufikiri ukubwa wa Goliathi, lakini alisimama imara hadi pale ushindi ulipopatikana. Huo ndio unapaswa kuwa mkao wako wa kutokata tamaa kamwe unapokabiliwa na hali fulani.

## UKIRI WA KINABII

**Nimezaliwa na Mungu, mimi ni mshindi, sitakata tamaa wala kujisalimisha. Tumaini langu liko kwa Kristo hadi nione matokeo ninayotamani katika mwaka huu wa Maajabu bila Idadi. Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 103:5




**BECOME A UAF PARTNER TODAY BY VISITING**
**WWW.UEBERTANGELFOUNDATION.ORG**

**UEBERTANGEL**
FOUNDATION





**Zaburi 69:9**
**"Maana wivu wa nyumba yako umenila, na laumu zao wanaokulaumu zimenipata."**

Mara nyingi Wakristo wengi huanza mtembeo wao wa Kikristo wakiwa wamechangamka sana na wamejaa nguvu za kuwa tu katika uwepo wa Bwana. Hawataacha kamwe hata ibada, kusanyiko au mkutano mmoja. Wao ndio wa kwanza kuwa pale mlango wa Kanisa unapofunguliwa, mapigo ya moyo kwa ajili ya Mungu yanakuwa ya juu zaidi, wakianza mtembeo wao wa Kikristo kama mbio za masafa mafupi.

Jambo la kusikitisha ni kwamba, jinsi mbio zinavyozidi kuwa ndefu na siku kugeuka wiki, wiki hadi miezi na miezi kuwa miaka, wanaanza kupungua. Sasa wanatoa visingizio, mahudhurio yao ya kanisani yanakuwa hafifu na ya kawaida. Mwali wa moto ndani yao sasa unakaribia kuzima. Hii ni hali mbaya sana kuwa nayo hasa katika nyumba ya Bwana. Biblia inatuambia katika (Mathayo 5:14) kwamba ''ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauweizi kusitirika ukiwa juu ya mlima.''

Leo, acha shauku hiyo kwa Kristo ndani yako iamshwe tena ili kuonyesha utukufu wake. Umekusudiwa ukuu, na ukuu huo upo ndani yako pale tu ulipompokea Yesu kama Bwana na Mwokozi wako. Yesu hajawahi kubadili nia yake juu yako, ni wakati wa kuwasha tena ule moto wa Roho Mtakatifu ndani yako.

## UKIRI WA KINABII

**Maisha yangu yatang'aa ili kudhihirisha nguvu za Roho Mtakatifu ndani yangu. Siwezi kufadhaika; Mimi si mtu niliyetupwa. Mimi ni ndani ya Kristo na Kristo yu ndani yangu. Maisha yangu yatang'aa zaidi na zaidi na zaidi kuonyesha utukufu wake. Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Yohana 2:17

# HAKUNA TENA WAKATI WA KULALA!



**Mathayo 13:25**
**"Lakini watu walipolala, akaja adui yake akapanda magugu katikati ya ngano, akaenda zake."**

Hebu fanya hesabu, kama ukilala masaa nane kila siku kama wanavyoshauri madaktari wengi ili upate mapumziko, ina maana unapofikisha umri wa kustaafu wa miaka 65 ulioidhinishwa na serikari nyingi, unaweza kuwa umelala kwa karibu miaka minane ya maisha yako! Hukugundua kuwa usingizi unakunyima mambo mengi sana. Katika andiko hili, adui hakupanda magugu wakati mpanzi akiwa macho wala adui hakuonekana wakati Mpanzi alipokuwa macho na kupanda. Adui alianza kupanda mbegu zake zenye kufisha wakati mwenye shamba akiwa amelala! Sasa unaweza kuona wazi kuwa usingizi ni lango la kumpa adui nafasi ya kuingia shambani kwako, kwenye biashara yako, kwenye fedha zako, kwenye ndoa yako, kwa watoto wako, kwa mwenzi wako, kwenye kazi yako!

Tatizo tulilonalo kanisani ni la wakristo wengi kulala, wengine wanalileta hata kanisani! Katikati ya huduma mubashara ya kanisani, wataenda kando kukaa ili kulala, bila kuwa na ufahamu wa mazingira yao! Kuhakikisha kuwa kila hali katika nyumba yako iko katika mpangilio sawa ni jukumu lako kama kuhani wa nyumbani kwako! Biblia inaweka hivyo katika (Mithali 6:10-11) ''bado kulala kidogo, kusinzia kidogo, Bado kukunja mikono upate usingizi; hivyo umaskini wako huja kama mnyang'anyi na uhitaji wako kama mtu mwenye silaha''. Kweli ni wakati wa kutolala tena! Amina.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mvunja vizuizi, mimi ni mvuka mstari, mimi ni mshindi, na si muhanga. Sitautumbuizia tena usingizi bali nitaufungia mpaka nitakapomaliza kazi yangu niliopewa na Mungu! Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 127:2



**Yohana 15:13**
**"Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake"**

Alichokifanya Yesu kwa ajili ya wanadamu, kwa kuutoa uhai wake kinatofautisha zile zinazoitwa dini za ulimwengu na Ukristo ambao kimsingi si dini. Upendo wa namna hii unaonyesha jinsi baba anavyowajali watoto wake.

Biblia inatuambia kwamba ''.....Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi'' (Warumi 5:8). Aina hii ya upendo kama ilivyoonyeshwa na baba, yapasa kuvuta umakini wetu katika mwenendo wetu wa Kikristo. Huu ndio udhihirisho wa upendo unaotarajiwa miongoni mwa Wakristo, upendo wako kwa ndugu na dada unapaswa kuakisi aina ile ile ya upendo ulioonyeshwa na Yesu na si wa mpaka vigezo fulani kutimizwa.

Unapomwona kaka yako au dada yako anapotoka au kupungukiwa mahali fulani au katika jambo fulani, marekebisho yako yanapaswa kufanywa tu sawa sawa na upendo huu wa ''agape''. Sisi ni kielelezo cha Kristo na nyaraka zilizoandikwa, na tunahitaji kufanya kazi kama Kristo. Upendo wa kweli unapaswa kufunika mwingiliano wetu na waamini wenzetu na wale wasioamini pia. Hakuna nafasi tena ya chuki, hasira, umbeya na kusengenyana. Acha upendo utiririke kutoka kwenye mazungumzo yako na kwa kufanya hivyo, roho nyingi zitavutwa kwa Kristo. Kristo ndiye kielelezo cha upendo wa kweli,na tunahitaji kuiga hilo.

## UKIRI WA KINABII

**Upendo unaotoka kwangu ni kamili, halisi, na safi; hakuna ajenda iliyofichika katika mtazamo wangu kwa wengine. Ninaendesha mambo kama Kristo; Mimi ni mbeba upendo wa agape na maisha yangu yataendelea kuchanua katika jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Yohana 3:16



**Hebreus 4:12 (NVI)**
**Waebrania 4:12**
**"Maana neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta, yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo."**

Mtu anastaajabu pale anaposoma andiko hili kwa kuwa limebeba mambo mengi sana. Je, ni aina gani ya teknolojia ambayo Mungu hutumia kugawanya nafsi na roho? Je , ni mbinu gani inatumika kwa kutoboa viungo na uboho? Neno la Mungu kulingana na maandiko ni ''hai''; linapumua, linaona, linasonga, linafikiri. Hii ina nguvu, hasa jinsi Neno la Mungu linavyochukuliwa kuwa si kitu, kwa Maandiko kusema haya yote kuhusu Neno la Mungu ina maana kwamba tunapaswa kufikiri upya juu ya mwenendo wetu kuhusiana na  Neno la Mungu. Kutokana na kile tunachojua Neno la Mungu hufanya, inamaanisha tunahitaji kuliheshimu Neno la Mungu. Neno la Mungu peke yake ni ghala la silaha, jeshi lililo imara na lenye silaha za kuleta maangamizi katika kambi ya adui.

Si ajabu kwa nini Yesu katika makabiliano yake na shetani alitumia Neno la Mungu kwa kusema kila mara . ''Imeandikwa'' katika kujilinda na kuvamia kwake. Vita za kimwili unazokabiliana nazo zina tafsiri ya kiroho inayopaswa kushungulikiwa kwa kutumia silaha za mizinga za kiroho . Ikiwa Bwana wetu Yesu alikabiliana na adui mkuu kwa Neno la Mungu na kupata ushindi, kwa nini unafikiri utapata ushindi katika biashara yako na maisha ya familia bila Neno la Mungu? Ni wakati wa kusema Neno leo!

## UKIRI WA KINABII

**Ninakingwa katika Neno lake, ninalindwa na Roho yake, naam, Kristo ndani yangu tumaini la Utukufu. Sitashindwa kamwe. Maisha yangu daima yataenda juu katika Kristo katika jina la Yesu, Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Waefeso 6:17



**Mwanzo 1:28**
**"Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi"**

Wooow! Mwongozo wa maelekezo ya Mungu kwa mwanadamu umeandikwa katika andiko hili. Kila kitu kinachohitajika kwa mwanadamu kufanya kazi na kutawala kiliingizwa ndani yake na maneno haya kama yalivyonenwa na Muumba. Sasa unaweza kuona kwa nini nasema mara nyingi kwamba, thamani yangu inafafanuliwa na maneno ninayozungumza na si kwa maoni ya mtu mwingine yeyote kunihusu? Inaenda kwa kila muumini . Umepewa mamlaka juu ya kila kitu, vinasaba vya kuzaa, kuzidisha na kujaza vimepachikwa ndani yako. Mungu anakuweka juu ya uumbaji na kukupa uwezo wa kutawala.

Wewe ni teknolojia ya Mwenyezi ambaye umejaliwa uwezo kama huo wa kutiisha . Kwa hiyo, uhaba unapaswa kutokuwa sehemu ya maisha yako kwa sababu una uwezo uliopewa na Mungu wa kujizalisha na kurekebisha sehemu ya maisha yako iliyoharibika. Unapochunguza maisha yako na kugundua kuwa hakuna kuzaa na kuongezeka, basi unajua kuwa umefikia hatua ya kutofanya kazi vizuri. Unapofanya vibaya, acha kutafuta suluhisho mahali pengine kwani unayo teknolojia iliyojengwa ndani ya kugundua makosa yako na kutoa suluhisho katika Neno la Mungu. Mara tu unapoamshwa na ukweli huu wa wewe ni nani, ni bora kwako kutumia mamlaka.

## UKIRI WA KINABII

**Ninafanya mambo kama Mungu . Mimi ni makao makuu ya Mungu BABA na maisha hayawezi kubanwa kutoka kwangu . Ninaweza kurekebisha makosa yangu na kujitengenezea upya wa maisha ndani yangu. Mimi ni mshindi na juu ya hali zote.**

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Wakorintho 9:27



**Waefeso 2:10**
**"Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo."**

Kazi ya Mungu iliyoumbwa katika Kristo Yesu inadokeza kazi kuu ya Mungu. Mungu alitumia muda wake wa thamani kukufinyanga. Wale ambao wamezoea kutengeneza matofali kwa njia ya zamani watapata ulinganisho huu vizuri.

Katika mchakato wa kutengeneza matofali , kuna utumiaji wa mtambo wa kufinyanga unayotumika kufyatua umbo la tofali zinazopaswa kutengenezwa. Mtambo huo, hutumiwa kila wakati kwenye matofali katika muundo au umbo lile lile kufyatua tofali lililo na picha ya tope hilo. Hivyo ndivyo tulivyo katika Kristo. Tumeumbwa kwa mfano wa Mungu, tukiwa na utendaji wa kufanya kazi katika sura ya Mungu, kufanya mambo ambayo Mungu atafanya haswa. Maandiko ya leo yanaisha na ''...ili tuenende katika hayo'' . Matendo haya mema yaliyotayarishwa kabla, ni wangapi kati yetu wanaoenenda katika hayo?

Madhihirisho ya nguvu kutoka juu ni sehemu ya pakacha hili lakini ni Wakristo wachache sana wanaotembea katika nguvu hizo. Umeingiziwa DNA ya Mungu na kutengwa kuwa ishara na maajabu kwa kizazi chako, lakini hakuna anayekujua. Nguvu inayokaa ndani yako imelala , vinginevyo uanze kuitumia hiyo nguvu, haitakufaidia chochote. Vinginevyo, uanze kuitumia hiyo nguvu ya Mungu iliyo ndani yako, maisha yako hayatadhihirisha utukufu wake, Mungu ameshakupa nguvu, imebaki kwako kutenda.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mfano mtukufu wa Mungu, nimeungwa mbinguni na kusambazwa kwa ulimwengu. Maisha yangu daima yataonyesha tabia na asili ya Mungu. Ninabeba DNA ya Mungu na nitakuwa Mkristo wa kutoa uthibitisho daima, kwa jina la Yesu ! Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Isaya 19:25



**Mathayo 25:16**
**"Mara yule aliyepokea talanta tano akaenda, akafanya biashara nazo, akachuma faida talanta nyingine tano."**

Nampenda huyu jamaa katika aya hii. Biblia inatuambia kwamba mara tu alipopokea talanta tano, hakukawia bali aliwekeza mara moja. Alianza kununua na kuuza bidhaa . Alikuwa kwenye soko la hisa kama ilivyo biashara yoyote halali na hakungoja kuambiwa cha kufanya. Wakristo pekee ndio watasubiri na kungoja, wakiwaambia watu, wanamngojea Bwana wakati kwa kweli Bwana anawangojea wao kupiga hatua hiyo ya kimkakati.

Unafikiri ni nani aliyekupa wazo hilo? Uliunganishwaje na rasilimali? Nani anaweka hiyo hamu na moto wa kuingia kwenye biashara kuwaka ndani yako? Kufikia sasa, unapaswa kujua kwamba ni kazi ya Bwana. Tayari amekwisha anza kazi ndani yako . Ni lazima ufahamu hili na uanze kuhamia maeneo ambayo hayajatengwa bado. Ni wakati wa kuanza biashara hiyo ambayo umetamani kwa muda mrefu na kunyoosha wavu wako hadi kilindini. Umekuwa ukivua katika maji ya kina kifupi kwa muda mrefu na sasa ni wakati wa kusonga mbele zaidi. Umekuwa wa kiwango cha chini sana kwa muda mrefu, sasa ni wakati wa kwenda kimataifa, haswa kutokana na ujio wa majukwaa haya mapya ya mitandao ya kijamii. Leo, unaposukumwa katika Roho, usitulie. Mwenzetu katika maandiko ya leo alichukua hatua mara moja na akapata faida asilimia mia moja, ambayo inapaswa kuwa mtazamo wako.

## UKIRI WA KINABII

**Maisha yangu yanafurahia manufaa ya kila siku kutoka kwa Mungu, na ninaitwa kwenye ukuu. Mimi nina mfadhili wa ufalme na sumaku ya fedha; kuchelewa hakupo kwenye msamiati wangu. Nitafanikiwa kwa kila nifanyalo kwa jina la Yesu. Amina.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Warumi 12:6



**Marko 1:41**
**"Naye akamhurumia, akanyosha mkono wake, akamgusa, akamwambia, Nataka, takasika."**

Ili Mungu akutumie kuponya wagonjwa unahitaji kuguswa na hali mbaya, mahitaji, na madhaifu ya wengine. Chembe ya huruma ipo, lakini inahitaji mguso papo hapo kwanza. Kusukumwa hufanya jambo lisiloelezeka litaharakishwe rohoni mwako unapoona au kumkaribia mtu mwenye maumivu. Ni kama kusikia maumivu ya mtu anayehitaji uponyaji.

Mara unapopata mguso, papo hapo unajifungua ili kufikia kiwango kingine cha neema ambapo uponyaji huanza kutiririka kwenye mwili wako hadi kwenye upeo wako wa mateso kisha unapowagusa wagonjwa, wanapona. Ikiwa hakuna mguso ndani yako ambao utaendana na hali mbaya ya mtu na kuumba mazingira ambapo nguvu za Mungu zitatiririka, basi umeanza zoezi lisilofaa.

Mungu anauona moyo wako unapowakaribia viziwi, bubu, vipofu, mwenye saratani au VVU. Msukumo wa kutaka kumuona mgonjwa akiponywa, Mungu kwa Roho wake huachilia nguvu za kuponya na hivyo ndivyo inavyofanya kazi. Usijaribu kutamka uponyaji katika maisha ya mtu kwa jina la Yesu, wakati haujaguswa hata kidogo. Itakuwa tu mojawapo ya mapokeo ya kidini ambayo hulifanya Neno la Mungu kuwa bure.

## UKIRI WA KINABII

**Upendo wa Mungu umemiminwa ndani ya moyo wangu. Moyo wangu unakubali kuguswa na mahitaji ya wengine. Nitakuwa baraka kwa wale wanaonizunguka na kwa wale ambao nakutana nao!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Luka 7:13



**Mathayo 6:21**
**"Kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako."**

Unapoona mstari huu katika Biblia yako ukiwa na alama ''nyekundu'', inamaanisha, Bwana wetu Yesu mwenyewe alisema maneno haya. Ukiweka pesa zako kwenye kamari, mbio za farasi, au matokeo ya michezo kama tenisi, mpira wa miguu, raga, au mpira wa vikapu, basi moyo wako hakika utakufuata huko. Watazamaji wa michezo hii wameweke-za pesa huko, kwa hivyo wana shauku na nia kubwa ya kuwa huko. Maneno ya Bwana wetu, Yesu yatakuwa ya kweli daima, vivyo hivyo unapoweka fedha zako Kanisani, moyo wako utafuata.

Wakristo wengi wakati mwingine huchukua uamuzi wa makusudi wa kutotoa sadaka achilia mbali kutoa zaka, sababu wanayotoa ni mchungaji atazila! Wanataka kumchezea Mungu linapokuja suala la fedha zao, wakisahau kwamba yote yako machoni pa Bwana kukuona na kukupa thawabu . Una wajibu wa kuunga mkono kazi ya Mungu na hilo linafikiwa kupitia utoaji wako. Baadhi ya watu ni wabahili kiasili na wanajulikana kwa hilo katika familia zao . Watauliza kila thumuni na senti kutoka kwa wenzi wao , ni kiasi gani zaidi kanisani. Tabia hii ya kuzuilia fedha zako ukijua kwamba kanisa litakuwa na uhitaji kwa kuwa Habari Njema lazima ihubiriwe katika pembe nne za dunia ina madhara kwako mwenyewe. Unapoachilia kile kilicho mikononi mwako kwa ajili ya kazi ya Mungu, atakufungulia fursa za kuziongeza fedha zako kwa njia ambazo huwezi kufikiria.

## UKIRI WA KINABII

**Ninapomtolea Mungu, ninapanda katika maisha yangu ya baadaye, kile ninachokiachilia kwa Mungu hakipotei kamwe. Ninapopanda katika huduma hii, ninapanda kwenye udongo wenye rutuba na mavuno yangu mengi yamehakikishwa . Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mithali 23:4



**Luka 17:1**
**"Akawaambia wanafunzi wake, Makwazo hayana budi kuja..."**

Somo hili la ''makwazo''au ''kukwazwa'' ni nyeti sana na limekita mizizi ndani ya mwili wa Kristo. Haliwezi kuisha katika mistari au aya chache kwani linapita mipaka mingi. Viongozi wa kanisa wanaudhika au kukwazika; washirika wa kanisa nao pia huchoka na kanisa kwa sababu wanakwazwa na ndugu au dada wenzao katika Bwana.

Nyakati fulani, inakuwa vigumu kumwambia ndugu au dada ukweli wa dhati kwa sababu wanakwazika kirahisi hata kama ni kwa manufaa yao wenyewe. Muumini wa kweli lazima awe na roho inayofundishika ili kukubali kusahihishwa na kupokea karipio la uaminifu kwa ajili ya kuboresha maisha yake. Ukiamua kutobadilika kamwe, 'ole itakujia'. Makwazo ni kama mtego unapouangukia, utanaswa. Kamwe usikwazike kwa mambo madogo au mambo ya upuuzi, yataitafuna tu nafsi yako kwa uchungu. Acha makwazo hayo yagonge mwamba na uchague kuwa na furaha mbele ya majaribu.

Katika (Mithali 18:19), tunasoma ''Ndugu aliyechukizwa ni mgumu kuliko mji wenye nguvu; Na mashindano ni kama mapingo ya ngome'' Usiwe mtu wa kulitimiza andiko hili! Jifunze kusamehe unapokwazika na usiwe ndiwe wa kusababisha makwazo!

## UKIRI WA KINABII

**Siwezi kukwazika kwa urahisi kama mtoto wa Mungu. Moyo wangu ni thabiti kwa BWANA na sitaondoshwa na makwazo bila kujali ukubwa wake. Siku zote nitasimama imara katika Kristo na kutangaza ushindi juu ya kila kwazo katika jina kuu la Yesu . Amina!**

**MAFUNZO ZAIDI**
1 Petro 2:23



**1 Wakorintho 3:6**
**"Mimi nilipanda, Apolo akatia maji; bali mwenye kukuza ni Mungu."**

Aya ya leo inazungumzia vipengele vitatu vya msingi vya mchakato wa kilimo: kupanda, kumwagilia na kukuza. Mbili za kwanza zinafanywa na wanadamu, ya mwisho ni Mungu pekee ndiye anayefanya. Unaposikia na kuona matawi ya kanisa yakichipuka katika kila mji, nchi, na bara, unapaswa kufurahia na kusherehekea. Pengine, upandaji umefanywa kabla ya wewe kufika kwenye eneo la tukio, lakini hiyo haikuzuii kumwagilia. Kumwagilia kile kilichopandwa hakuhitaji ujuzi maalum. Ikiwa unafurahishwa na huduma ya watoto katika tawi la karibu, basi jitolee kuhudumu hapo. Ikiwa ni kuimba, basi sajili shauku yako na timu ya kusifu na kuabudu au kwaya, au kama ni ukarimu basi jiunge na wahudumu wa kanisa, n.k.

Chochote unachotaka kufanya katika nyumba ya Bwana ili kumwagilia shamba lake la mizabibu, iko nafasi kwa ajili yako. Kuna eneo moja ambapo kila mtu anakaribishwa, nalo ni utoaji ili kuhakikisha kwamba Habari Njema inaenea duniani kote na makanisa mengi zaidi yanapandwa : kwa njia hiyo unahusika katika kupanda. Kutoa visingizio sio chaguo, unakidhi vigezo! Mungu anakutarajia uwe mwenye bidii kwenye huduma . Una karama, kipaji,na uwezo wa kufikia kimo hicho katika Kristo.

## UKIRI WA KINABII

**Hakuna kazi ambayo siwezi kuifanya kupitia Roho Mtakatifu ndani yangu. Nina wito na karama ya kushiriki kikamilifu katika kazi ya Bwana. Siwezi kamwe kukaa wala kunyamaza tena, sasa nimejaa nguvu za kutangaza Habari Njema! Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Matendo 18:4



**Marko 11:23**
**"Amini, nawaambia, Ye yote atakayeuambia mlima huu, Ng'oka , ukatupwe baharini; wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini ya kwamba hayo asemayo yametukia; yatakuwa yake."**

Waumini wengi wamesoma mstari huu wa Biblia kwa kuurudia rudia lakini bado, hawajapata matokeo yanayotarajiwa. Inaonekana kuna kitu kinakosekana katika ufahamu wa kimsingi wa aya hii. Leo, nataka kutilia mkazo  kwenye ''wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini'' kwani huu ndio ufunguo wa kuwa na chochote unachosema. Kutokuwa na mashaka na kile ambacho Mungu anasema katika Neno lake kitaamua kuondolewa kwa mlima mbele yako. Je, umeona kwamba Yesu alizungumza kuhusu ''mlima huu'' , ambayo ina maana kwamba mlima hauko mbali nawe? Mlima huu unaweza kuwa changamoto zako za kifedha, masuala ya afya yako, ukuaji wako wa kiroho n.k. Kitu ambacho unahangaika nacho kwa sasa ni mlima anaouzungumzia Mungu. Hazina yako kuu katika kupata ushindi unaohitaji iko katika kuamini kabisa kile unachosema kwa kuwa na mashaka asilimia sifuri.

Anza kupanua upeo wako na mchakato wa mawazo uliobatilishwa kabisa kwa mashaka na kutoamini. Unapotambua hili na kuanza kutilia shaka mashaka yako, unapoamuru na kutangaza juu ya hali na mazingira katika maisha yako, matokeo yaliyokusudiwa yatazalishwa kwa jina la Yesu!

## UKIRI WA KINABII

**Moyo wangu hauna shaka, kwa hivyo, chochote ninachofanya, chochote ninachotamani, kitatokea katika maisha yangu. Ninatupa kila inchi ya mashaka mbali na maisha yangu milele. Haleluya!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 21:21



**Luka 9:57**
**"Nao walipokuwa wakienda njiani, mtu mmoja akamwambia, nitakufuata kokote utakakokwenda."**

Andiko hili ni muhimu sana kwa kila mtu anayejiona kuwa mwamini au asiye mwamini . Iwe uko katika huduma sasa hivi au la, ni kwa ajili ya wafuasi wote wa Kristo na wale wafuasi muhimu. Jina la mtu katika maandiko halikutajwa, Biblia inasema tu mtu mmoja, lakini tunajua kweli ilifanyika. Mtu huyu alijitolea kumfuata Yesu. Mara nyingi, Wakristo wengi na waenda kanisani wanangoja kuombwa kufanya kazi ambazo wanajua wana utaalamu nazo ndani ya kanisa.

Sisi sote tumeitwa katika huduma na kwa hivyo tunapewa karama fulani, vipaji, au uwezo ambao ukitumika utalifanya kanisa la Mungu kusonga mbele. Kusitasita au kungoja kuitwa ni hali inayolizunguka kanisa, inapunguza kasi ya maendeleo ya injili . Kwa wengine , ni hatua ya kimahesabu na ya kukusudia, wakati kwa wengine ni woga. Bila kujali kambi unayodondokea, mada kuu hapa ni kukwepa huduma . Tumeitwa kwenye utumishi, askari katika jeshi la Bwana, linalohitaji sisi kuwa hai na tunawaka moto kwa ajili ya Yesu. Siwezi kufikiria mtu yeyote anayeungua moto ambaye atatulia kimya tu, hilo haliwezekani kabisa! Mtu huyo atakimbia haraka kutafuta njia za kuuzima moto huo. Kwa hiyo, na tukimbie na agizo hili la ajabu ambalo Mungu ametupa leo!

## UKIRI WA KINABII

**Sasa ninawaka moto kwa ajili ya Yesu, hapana adui wa kuniweka chini . Maisha yangu yatang'aa kwa uzuri na kuvutia wengine kumuona Kristo ndani yangu. Siwezi kuionea aibu Injili kwa maana ni uweza wa Mungu dhidi ya adui.**

**MAFUNZO ZAIDI**
Mathayo 8:22



**Matendo 3:1**
**"Petro na Yohana walikuwa wakikwea pamoja kwenda hekaluni, saa ya kusali, saa tisa."**

Wanafunzi wa Yesu baada ya Yesu kupaa mbinguni walivaa vazi hatari linaloitwa ''MAOMBI". Watu hawa walivutiwa sana na maombi kiasi kwamba ikawa mfumo wao wa maisha. Siku zote walikuwa katika hali ya maombi hadi wakataja masaa fulani ya siku kuwa ''masaa ya maombi'. Ilikuwa maisha ya kila siku na ya kawaida kwao, si ajabu waliupindua ulimwengu juu chini katika zama zao. Kumbuka kwamba maombi ni mwamba na msingi wa Ukristo. Ikiwa unaweza kupata muda wa kula, basi unapaswa kupata muda wa kuomba. Biblia inatuagiza hasa kwamba ''... inatupasa kuomba siku zote wala tusikate tamaa'' (Luka 18:1).

Waumini wengine watasema, sijui jinsi ya kuomba. Unapokuwa hujui nini cha kuomba na jinsi ya kuomba, ni wakati wa kumuomba Roho Mtakatifu. Atakufundisha lugha yake ambayo ni kunena kwa lugha ambayo zinaeleweka kikamilifu na Mungu, lakini akili yako ya asili haitaelewa. Unapoomba kwa lugha ya Roho Mtakatifu, Roho Mtakatifu atafanya maombezi kwa ajili yako. Mambo ambayo unaweza kuwa umeyachukulia kawaida katika maisha yako, katika biashara yako, katika familia yako, na katika mtembeo wako wa kiroho yataombewa huku Roho Mtakatifu akitawala kipindi chako cha maombi na kukuombea sawa sawa na mapenzi ya Mungu. Usipuuze maisha yako ya maombi kwa sababu hiyo ndiyo yanayokutegemeza kama Mkristo. Kuwa makini kuhusu maisha yako ya maombi leo!

## UKIRI WA KINABII

**Sasa ninabadilisha gia katika maisha yangu ya maombi. Siwezi kuishi maisha yasiyo na maombi. Mimi ni mtoto wa Mungu na ninajua njia pekee ya kuwasiliana na Baba ni kupitia maombi. Amina!**

**MAFUNZO ZAIDI**
Zaburi 55:17



# HAVE YOU RECEIVED JESUS CHRIST YET?

WE INVITE YOU TO MAKE JESUS CHRIST THE LORD OF YOUR LIFE BY PRAYING THIS PRAYER;

"O LORD GOD, I COME TO YOU IN THE NAME OF JESUS CHRIST. I BELIEVE WITH ALL MY HEART IN JESUS CHRIST, SON OF THE LIVING GOD. I BELIEVE HE DIED FOR ME AND GOD RAISED HIM FROM THE DEAD. I BELIEVE HE'S ALIVE TODAY. I CONFESS WITH MY MOUTH THAT JESUS CHRIST IS THE LORD OF MY LIFE FROM THIS DAY. THROUGH HIM AND IN HIS NAME, I HAVE ETERNAL LIFE; I'M BORN AGAIN. THANK YOU LORD, FOR SAVING MY SOUL! I'M NOW A CHILD OF GOD. HALLELUIAH!"

CONGRATULATIONS! YOU ARE NOW A CHILD OF GOD.

TO RECEIVE MORE INFORMATION ON HOW YOU CAN GROW AS A CHRISTIAN, PLEASE GET IN TOUCH WITH US ON

UK: +44 3333 448 612
USA +1 240 781 6942
RSA +27 51 004 0209

WWW.UEBERTANGEL.ORG | WWW.GOODNEWSWORLD.COM

# SCRIPTURE PASSAGE FOR PROTECTION

## ISAIAH 54:


14 I AM BUILD SOLID, GROUNDED IN RIGHTEOUSNESS,
FAR FROM ANY TROUBLE—NOTHING TO FEAR!
FAR FROM TERROR—IT WON'T EVEN COME CLOSE!

15 IF ANYONE ATTACKS ME,
I WILL NOT THINK FOR A MOMENT THAT GOD SENT THEM,
AND IF ANY SHOULD ATTACK ME,
NOTHING WILL COME OF IT.

16 GOD CREATED THE BLACKSMITH
WHO FIRES UP HIS FORGE
AND MAKES A WEAPON DESIGNED TO KILL.
HE ALSO CREATED THE DESTROYER—

17 BUT NO WEAPON THAT CAN HURT ME
HAS EVER BEEN FORGED.
ANYONE WHO ACCUSES ME
WILL BE DISMISSED AS A LIAR.
I AM GOD'S SERVANT SO THIS IS WHAT I CAN EXPECT
GOD WILL SEE TO IT THAT EVERYTHING
WORKS OUT FOR THE BEST FOR ME."

THIS IS WHAT GOD SAYS TO ME AND IT WILL NOT FAIL IN JESUS'S NAME!



The Good News World Helplines

USA: +1 (240) 781-6942

UK: +44 333 344 8612

RSA: +27 (51) 004-0209

www.goodnewsworld.com